MIMI NI RAFIKI WA ELIMU

Mimi ni Rafiki wa Elimu

Mhariri: John Kalage
Waandaaji: Naomi Mwakilembe, Pius Makomelelo, Joyce Mkina, Honoratus Swai na Agnes Mangweha
Wachangiaji: Robert Mihayo, Elisante Kitulo, Presscodd James
Mchoraji: Ramadhani Msuya

ISBN 978-9987-18-054-7

© HakiElimu, 2017
SLP 79401, Dar es Salaam, Tanzania
Barua pepe: info@hakielimu.org
Tovuti: www.hakielimu.org

Sehemu yoyote ya kitabu hiki inaweza kunakiliwa kwa minajili isiyo ya kibiashara; ilimradi chanzo cha sehemu iliyonakiliwa kinaonyeshwa na nakala kutumwa kwa HakiElimu.

Utangulizi

Karibu! Hongera kwa kuwa *Rafiki wa Elimu*. Wewe ni mmoja wa wanaharakati wengi ambao wanajali elimu na demokrasia Tanzania! Ni wajibu wako kushiriki kikamilifu kuleta mabadiliko!

Kitabu hiki kimetengenezwa kwa ajili ya *Marafiki wa Elimu* kama rejea katika shughuli zao za kila siku. Kinatoa maelezo mafupi kuhusu Harakati za *Marafiki wa Elimu* ili kupanua uelewa wa walengwa kuhusu historia, madhumuni na uendeshaji wa Harakati hizi. Pia kinatoa maelezo kuhusu haki na wajibu wa *Rafiki wa Elimu* katika Harakati.

Tunataraji kwamba kitabu hiki kitajibu maswali mengi ambayo unaweza kuwa nayo kuhusu Harakati za *Marafiki wa Elimu* na kukutia hamasa zaidi kushiriki kikamilifu katika harakati za kuleta mabadiliko katika utoaji wa huduma ya elimu nchini. Kama una maswali zaidi kuhusu Harakati hizi tafadhali wasiliana nasi, tutajitahidi kukujibu.Vilevile kama una maoni ya kuboresha kitabu hiki tafadhali tuandikie.

NI JAMBO ZURI KUJIUNGA NA HARAKATI HIZI ZA MARAFIKI WA ELIMU ILI KUSAIDIA ELIMU HAPA KIJIJINI KWETU
OFISI YA KIJIJI
TANGAZO
MARAFIKI WA ELIMU

ANAJAZA FOMU YA KUJIUNGA NA HARAKATI...
HARAKATI HIZI ZITAKIDHI KIU YANGU YA MUDA MREFU YA KUSHIRIKI KATIKA KUBORESHA ELIMU..
MASHARTI YA KUJIUNGA

BAADA YA MUDA ANAPOKEA KIFUNGASHI CHA
TAARIFA ZA AWALI KUTOKA Haki Elimu..
POSTA

ANASOMA NA KUELEWA...
KWA KUTUMIA MACHAPISHO HAYA NAWEZA KUSAIDIA KUINUA ELIMU KATIKA KIJIJI CHETU...
LAKINI NGOJA NIWASHIRIKISHE PIA WATU WENGINE ILI NIPATE MAWAZO ZAIDI JUU YA ELIMU KWA WATOTO WETU

SASA NIMEELEWA VIZURI KUHUSU MARAFIKI WA ELIMU. LAKINI TUTAANZIA WAPI SISI WATU WA KAWAIDA KUCHANGIA KATIKA ELIMU?
HAPANA... NI WAJIBU WETU SOTE KUHAKIKISHA WATOTO WETU WANAPATA ELIMU BORA.. MIMI NAONA SUALA LA UTORO KWA WANAFUNZI LIMEKUWA KERO..
HATA TUKICHANGIA MAWAZO YETU NI BURE TU... HAWATA-YAFANYIA KAZI

ANATAFUTA MARAFIKI WENGINE WA ELIMU NA KUPEANA NAO MAWAZO ZAIDI...
NI KWELI UTORO NI CHANZO CHA WANAFUNZI KUFELI..
INABIDI TUSHIRIKIANE NA UONGOZI WA SHULE ILI TUBAINI NJIA NZURI YA KUWASAIDIA WANAFUNZI WETU
SAWA KABISA
VOCHA ZIPO

NIMEKAGUA MADAFTARI YA MWANANGU NIMEGUNDUA HAANDIKI IPASAVYO AKIWA SHULENI...
HATA MIMI NIMEFUATILIA KWA KARIBU...NI WAZI KUWA WATOTO WETU HAWAHUDHURII VIZURI DARASANI..KESHO TWENDE SHULENI TUONANE NA WALIMU WAO..

WANAELEKEA SHULENI KUPATA
MAELEZO ZAIDI KUTOKA KWA WALIMU...


WANAONGEA NA MKUU WA SHULE...
SISI NI MARAFIKI WA ELIMU.. TUNAPENDA KUSHIRIKIANA NANYI KUSAIDIA ELIMU KATIKA SHULE HII, HUSUSANI KATIKA UTORO KWA WANAFUNZI...
KARIBUNI SANA... WANAFUNZI WAME-KUWA WAKIKOSA MASOMO YAO MARA KWA MARA

UTORONI MIONGONI MWA MAMBO YANAYOHATARISHA UFAULU KWA WANAFUNZI.. SISI WALIMU NA WAZAZI LAZIMA TUSHIRIKIANE ILI KUDHIBITI TABIA HII..
NI WAZO ZURI SANA. TUWASHIRIKISHE WAZAZI TUJADILI PAMOJA
KWELI...WAZAZI WAKI-SHIRIKISHWA WATASAI-DIA KUDHIBITI UTORO TOKA NYUMBANI NA MITAANI.. AGENDA HII IPELEKWE KWENYE MKUTANO WA KIJIJI

MKUU WA SHULE ANAANDAA KIKAO CHA WAZAZI...
WAZAZI KARIBUNI..TUJADILIANE JUU YA TABIA YA UTORO KWA WANAFUNZI SHULENI...

NDUGU WAZAZI WATOTO WETU HAWAFIKI SHULENI MARA KWA MARA NA WANAZURURA MITAANI.. KILA MZAZI ANA WAJIBU WA KUMREKEBISHA MWANAFUNZI YEYOTE ANAYEONEKANA MITAANI MUDA WA MASOMO...
TUFUATILIE KILA SIKU MAENDELEO YA WATOTO NA KUWASILIANA NA WALIMU ILI KUFAHAMU MIENENDO NA TABIA ZAO KIKAMILIFU
KWELI.. TUSIWAACHIE WALIMU PEKE YAO

ANAANDIKA BARUA KWA MHARIRI KUTOA MAONI YAKE...
CHANGAMOTO ZA UFAULU
Mhariri,
Kufaulu shuleni inawezekana.
Wanafunzi wanafeli mitihani
kwasababu nyingi za binafsi
Kama vile utoro, me

ANAFUATILIA ZAIDI MAHUDHURIO YA WANAFUNZI SHULENI...
MAHUDHURIO YAME-ONGEZEKA... WAZAZI WANAFUATILIA KWA KARIBU MAENDELEO YA WANAFUNZI
HONGERA PIA KWA KUCHAGULIWA KUWA MJUMBE KWENYE KAMATI YA SHULE
AFRICA
ASANTE... HIYO NI HATUA NZURI


KIKAO CHA KAMATI YA SHULE..
NI VIZURI TUWAITE WATORO SUGU PAMOJA NA WAZAZI WAO TUONGEE NAO PAMOJA
TUWAANGALIE PIA WANAFUNZI WANAO-ISHI KATIKA - MAZINGIRA MAGUMU ILI TUWASAIDIE...
PIA TUHAKIKISHE WALIMU WANAFU-NDISHA IPASAVYO DARASANI

ANASIKIA KIPINDI CHA ELIMU REDIONI...
SHIRIKI NASI KUTOA MAONI JUU YA KUBORESHA ELIMU..
WAMETOA NAMBA YA SIMU ILI TUTOE MAONI YETU..NGOJA NISHAURI WATU KUTUMIA FURSA HIYO...
SOAP

ANASHIRIKI KIPINDI CHA REDIO...
JE, NI KWA NAMNA IPI WANANCHI WANAWEZA KUSHIRIKI KUONDOA UTORO WA WANAFUNZI SHULENI?
NDUGU MTANGAZAJI WANAFUNZI WANAPOTOROKA SHULENI HUISHIA KATIKA MAENEO YETU YA KILA SIKU... HIVYO KILA MWANANCHI ANA WAJIBU WA KUHAKIKISHA WANAFUNZI WANAKUWA SHULENI NA SIYO MITAANI


WANANCHI WANAPATA HAMASA..
NITOE WITO PIA KWA WANAFUNZI KUZINGATIA MASOMO YAO SHULENI MUDA WOTE..WALIMU NA WAZAZI TUHAKIKISHE TUNAZUNGUMZA NA WANAFUNZI ILI KUZITAMBUA CHANGAMOTO ZA KIELIMU ZINAZOWAKABILI KILA SIKU...
NI KWELI KABISA.. HAPA KWETU WATOTO HAWAZINGATII MASOMO KWASABABU YA VISHAWISHI HASA KWA WASICHANA
WAZAZI PIA TUWE MFANO MZURI KWA WATOTO

WATOTO NI WETU NA ELIMU BORA NI KWA AJILI YETU SOTE.. TUKIWASIMAMIA HAWATAYUMBISHWA
HATA SISI KAMA SERIKALI YA KIJIJI TUNAHAKIKISHA WANAFUNZI WANAKUWA SHULENI MUDA WOTE NA SIO VIJIWENI...
NI WAKATI SAHIHI SASA KUJIUNGA NA HARAKATI ZA MARAFIKI WA ELIMU

Mimi ni Rafiki wa Elimu!

Tarehe iliyopokelewa .....
Jina .....
Anwani ya Posta.....
Namba ya simu .....
Barua pepe .....

Jinsi ☐ Mme ☐ Mke

Umri
- ☐ 7 - 14
- ☐ 15 - 19
- ☐ 20 - 30
- ☐ 31 - 40
- ☐ Zaidi ya 41

Kiwango cha Elimu
- ☐ Elimu ya Msingi
- ☐ Elimu ya Sekondari
- ☐ Chuo

1. Kitabu hiki kina habari muhimu?	☐ Ndio	☐ Hapana	☐ Kiasi
2. Kitabu hiki kina manufaa?	☐ Ndio	☐ Hapana	☐ Kiasi
3. Kitabu hiki kinaeleweka kiurahisi?	☐ Ndio	☐ Hapana	☐ Kiasi
4. Kitabu hiki kinavutia?	☐ Ndio	☐ Hapana	☐ Kiasi
5. Kitabu hiki kimeandikwa vizuri?	☐ Ndio	☐ Hapana	☐ Kiasi
6. Umependa michoro ya kitabu hiki?	☐ Ndio	☐ Hapana	☐ Kiasi

HakiElimu inawezesha wananchi kuleta mabadiliko kwenye elimu na democrasia

HakiElimu
SLP 79401, Dar es Salaam, Tanzania
Barua pepe: info@hakielimu.org
Tovuti: www.hakielimu.org